## 4.0 KISWAHILI

Wakati huu tumechanganua matokeo ya Kiswahili ya mwaka wa ***2007*** huku tukiyalinganisha na ya miaka ya ***2004, 2005*** na ***2006***.

**Fahirisi 4: Matokeo ya Kiswahili KCPE ya miaka 2004 hadi 2007**

| | **2004** | | **2005** | | **2006** | | **2007** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** |
| | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** |
| Alama ya wastani | 23.88 | 15.85 | 30.23 | 18.06 | 29.89 | 18.32 | 25.51 | 16.99 |
| Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi | 24 | 14 | 32 | 20 | 33 | 18 | 26 | 16 |
| Alama ya juu iliyotuzwa | 50 | 40 | 50 | 39 | 50 | 39 | 49 | 39 |

Fahirisi hii inatuonyesha kuwa kwa upande wa lugha:

(i) Alama ya wastani imeshuka kutoka alama ***29.89*** mwaka wa 2006 hadi ***25.51*** mwaka wa 2007. Hii ni tofauti ya alama ***4.38***.

(ii) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi imeshuka kwa alama ***7*** kutoka ***33*** mwaka wa 2006 ikawa ***26*** mwaka wa 2007.

(iii) Alama ya juu iliyotuzwa ni ***49***. Alama hii ilikuwa ***50*** miaka yote minne iliyopita.

Kwa upande wa insha:


(i) Alama ya wastani imeshuka kutoka ***18.32*** mwaka wa 2006 hadi ***16.99*** mwaka wa 2007.

(ii) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi imeshuka kwa alama ***2*** kutoka ***18*** mwaka wa 2006 hadi ***16*** mwaka wa 2007.

(iii) Alama ya juu iliyotuzwa bado ni ***39***.

Mchoro huu unatuonyesha vile alama za sehemu za lugha na insha zilivyojitawanya.


Powered By: www.manyamfranchise.com




Mchoro huu unatuonyesha kwamba watahiniwa wengi waliweza kupata alama nusu ya alama zote zinazoweza kutuzwa katika sehemu ya lugha. Alama hizi ni ***25*** juu ya ***50***. Katika upande wa insha watahiniwa wengi hawakuweza kupata alama zaidi ya nusu ya alama zote ambazo zinaweza kutuzwa ambazo ni ***20*** juu ya ***40***.

## 4.1 SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

Mchoro huu unatuonyesha asilimia ya watahiniwa tuliochanganua ambao walipata jibu sawa katika kila swali.



Kila mwaka huwa tunachanganua maswali ambayo yaliwatatiza watahiniwa. Maswali hayo yalikuwa ya ***8, 17, 20, 34, 35, 47, 48*** na ***49***.

**FAHIRISI 5: Maswali ambayo yaliwatatiza watahiniwa**

| **Maswali** | **8** | **17** | **20** | **34** | **35** | **47** | **48** | **49** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliopata jibu sawa | 17.01 | 18.33 | 33.81 | 19.59 | 14.87 | 32.44 | 25.36 | 20.31 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 30.06 | 32.10 | 30.74 | 29.05 | 31.01 | 28.32 | 29.32 | 28.71 |

* Inaonyesha jibu sawa

Msichana alikuwa amechoshwa na vitimbi vya kasri __8__ shangazi yake ambaye alikuwa amemtoa kijijini kuja kumpeleka shule. __9__ alikuwa na nia ya kumfanya __10__ . Hakujua amlaumu shangazi yake huyu, __11__ majaliwa __12__ wazazi wake na kumwacha yatima. Alikumbuka jinsi __13__ na matumaini ya kusoma kwa bidii ili kuiokoa jamii __14__ kutokana na umaskini __15__ hali zao.

**Swali la 8:**

A. la B. ya C. mwa D. kwa

**Matokeo ya swali la 8**

| **Majibu** | ***A** | **B** | **C** | **D** |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 17.01 | 52.66 | 7.57 | 21.47 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 30.06 | 27.53 | 24.46 | 26.01 |

Katika kifungu cha maswali ya *8* mpaka *15*, panazungumziwa msichana ambaye anaishi katika jumba la shangazi yake. Jumba hili ni kasri yaani nyumba kubwa.
Swali hili limetahini mbinu ya ujuzi pamoja na ile ya matumizi.

Neno kasri liko katika ngeli ya ***li – ya***. Inaonekana watahiniwa wengi hawakuelewa maana ya neno kasri ama pengine kama walielewa hawakujua liko katika ngeli ipi. Jibu sawa lilikuwa ***A – la.***

**Swali la 17**

Kitenzi <u>nawa</u> katika kauli ya <u>kutendesha</u> ni:

A. nawika
B. nawia
C. navya
D. nawishwa

**Matokeo ya swali la 17**

| **Majibu** | **A** | **B** | ***C** | **D** |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 8.99 | 21.28 | 18.33 | 50.05 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 24.86 | 25.97 | 32.10 | 26.74 |

* Inaonyesha jibu sawa

Mbinu iliyotahiniwa hapa ni ya ujuzi.

***Nawika*** ni kauli ya ***kutendeka, nawia*** ni kauli ya ***kutendea*** na ***nawishwa*** ni kauli ya ***kutendeshwa***. Kwa hivyo jibu sawa lilikuwa ***C. Navya***, ambayo ni kauli ya ***kutendesha***.

**Swali la 20**

Chagua sentensi iliyo na kivumishi cha sifa.
A. Mwanafunzi ameandika insha nyingine.
B. Daktari amewatibu wagonjwa watatu.
C. Mpishi amepika chakula kibichi.
D. Mtoto yule anaweza kukimbia.

**Matokeo ya swali la 20**

| Majibu | A | B | *C | D |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 10.72 | 15.87 | 33.81 | 38.39 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 24.12 | 24.75 | 30.74 | 26.47 |

* Inaonyesha jibu sawa

Mbinu iliyotahiniwa katika swali hili ni ile ya uchanganuzi.

Inaonekana wafunzi hawajaielewa vyema dhana ya vivumishi. Sentensi za ***A, B, C, D*** hapa zote zina vivumishi tofauti. Katika ***A***,neno ***nyigine*** ni kivumishi cha pekee, katika ***B***, neno ***watatu*** ni kivumishi cha idadi, katika ***C***,neno ***kibichi*** ni kivumishi cha sifa na katika ***D***,neno ***yule*** ni kivumishi kionyeshi ama kiashiria. Kwa hivyo katika swali hili jibu lilikuwa ***C. Kibichi***

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 – 40.*

Nilizaliwa na kulelewa katika familia iliyotajika. Baba yangu Mlajasho alikuwa tajiri wa mali na moyo. Mimi na ndugu yangu mdogo hatukujua maana ya uhitaji kwani baba alitukidhia mahitaji yetu yote. Nyumbani mwetu kila siku mlishiba na kutapika watu wa kila sampuli waliokuja kulilia hali kwa baba. Baba aliwasabilia kwa mengi. Kuna waliopewa ruzuku mbalimbali za vyakula, kuna waliopewa vibarua mashambani na waliofanya kazi pale nyumbani. Almuradi kila mwana kijiji alifaidika kutokana na mkono wazi wa baba. Ndugu yangu mdogo hakuisha kuwabughudhi waja hawa na kuwaita waegemea nundu.

Siku zilisonga na kupita kama maji ya mto; hata nikajipata katika shule ya msingi. Niliyakumbatia masomo yangu kwa hamu kubwa. Sikuwa na wakati wa kufanya ajizi, kwani baba, pamoja na pato lake nono, hakuwahi kudekeza hisia za ugoigoi. Nasi ilibidi tufuate nyayo zake; kwani mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina. Nilifanya mtihani wangu wa darasa la nane na kuvuna nilichopanda. Asubuhi baada ya kutangazwa kwa matokeo ya mtihani huo, niliamshwa na sauti ya, "pongezi mwanangu," kutoka kwa baba. Baba alikuwa amebeba gazeti la siku hiyo, usoni amevaa tabasamu kubwa. Sikuamini maneno yake. Nilimnyang'anya gazeti na ikawa kweli mwenye macho haambiwi tazama. Nilikuwa mwanafunzi bora nchini. Nilijiunga na shule mojawapo ya kitaifa.

Siku nilipokivuka kizingiti cha lango la shule ya kitaifa ya Tindi ndipo maisha yangu yalipoanza kuingia ufa. Nilikutana na Tamasha, mwanafunzi mchangamfu na mcheshi. Alijitambulisha kuwa alisomea shule iliyokuwa jirani na ile yangu ya msingi. Urafiki shakiki ukazaliwa kati yake nami. Tukawa daima tunaandamana. Hayo hayakunitia shaka, kwani Tamasha alinihimiza kila mara nitie bidii masomoni. Hata hivyo, siku zilivyosonga ndivyo tabia yake halisi ilivyonibainikia.

Jioni moja Tamasha alikuja chumbani mwangu akiwa amebeba unga aliouita dawa ya homa. Aliniambia nijaribu kutibu homa ambayo ilikuwa imenikaba kwa siku ayami. Nami, kwa kutotaka kumvunja rafiki yangu, nikachukua unga huo na kuutia kinywani; ingawa kwa kweli mwalimu wetu alikuwa ametuonya dhidi ya kutumia dawa zozote bila maelekezo ya daktari. Unga huu haukuitibu homa yangu, ila ulinipa utulivu mkubwa wa akili, utulivu ambao sikuwa nimewahi kuushuhudia maishani.

Tamasha alifika chumbani mwangu usiku kunijulia hali. Alinipata nimejituliza juu ya kitanda changu. Alinisalimu na kukenua kama aliyetarajia jawabu fulani kutoka kwangu. Nilimweleza hali yangu naye akaniambia kuwa hivyo ndivyo dawa hiyo ifanyavyo kazi; kwamba amekuwa akiitumia kwa muda, hata nyakati za mtihani; naye hupata nguvu za kukabiliana na majabali yote. Alinielekeza kwa Mzee Kamaliza ambaye ndiye aliyekuwa akimuuzia unga huo. Kuanzia siku hiyo nikawa mteja mwaminifu wa Kamaliza. Nilitumia unga huu bila fikira nikidhani kuwa ilikuwa dawa ya homa tu! Sikujua ilikuwa dawa ya kulevya; na Tamasha alikuwa mraibu sugu wa dawa hiyo na nyingine nyingi! "Uzuri wake huu ni wa mkakasi tu?" Nilijiuliza. "Laiti ningalijua". Hata hivyo maswali yote haya hayakuwa na faida tena. Nilikuwa tayari nimezama katika tatizo sugu la matumizi ya dawa za kulevya.

Nilijisuta moyoni kwa matumizi ya dawa za kulevya ambayo yalielekea kuyagongesha mwamba maisha yangu shuleni. Hata hivyo, haikuwa rahisi kuacha kwani nilichelea kuitwa limbukeni na wenzangu. Matokeo ya haya yote yakawa kuzorota kwa masomo yangu. Walimu hawakuchelewa kuona mabadiliko yaliyonikumba. Walijaribu kunishauri na kutaka kujua kilichokuwa kikinisumbua. Walipoona kwamba hali yangu haibadiliki na kwamba nimeshindwa kuwaambia tatizo langu, walimjulisha mwalimu mkuu ambaye hakukawia kumwita baba.

Mazungumzo kati ya baba na mwalimu mkuu yalinitia fadhaa kubwa kwani sikutaka kuwaambia nilitumia dawa za kulevya; ingawa kwa kweli mwalimu mkuu alishuku. Walijaribu kunishika sikio kuhusiana na tabia hii yangu; lakini tangu lini sikio la kufa likasikia dawa? Niliendelea na uraibu wangu hadi siku nilipofumzwa na ulimwengu baada ya kufumaniwa na naibu wa mkuu wa shule mjini nikipiga maji. Nilipewa adhabu niliyotarajia. Nilijipata nyumbani kwa muda wa mwezi mzima, nikiuguza vidonda vya moyo na akili. Kijiji kizima kilijua nimefukuzwa shule kwa sababu ya matumizi ya dawa za kulevya. Sikuwa na pa kuutia uso wangu. Hata hivyo hili lilikuwa funzo kubwa kwangu.

Mama yangu aliweza kunipa nasaha na kunishauri niache kutumia dawa hizo. Mara hii, maneno aliyoniambia yalikuwa na maana. Niliyasikiliza kwa makini. Hata baba alipopata barua kumwarifu aniregeshe shule, nilikuwa tayari kurudi na kuyaanza maisha upya. Nilikuwa nimeamua kujiunga na chama cha vijana wanaopigana na matumizi mabaya ya dawa shuleni.

## Swahli la 34

Kifungu "ndipo maisha yangu yalipoanza kuingia ufa" kinamaanisha:

A. maisha ya msimulizi yalianza kupata matatizo
B. maisha ya msimulizi yaliporomoka.
C. maisha ya msimulizi yalianza kubadilika
D. maisha ya msimulizi yaliharibika

## Matokeo ya swali la 34

| Majibu | *A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 19.59 | 3.80 | 63.57 | 11.81 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 29.05 | 21.83 | 27.24 | 27.30 |

* Inaonyesha jibu sawa

Katika kutafuta jibu la swali hili, watahiniwa hawakuzingatia maana ya neno "***ufa***" ambalo ndilo neno lililoshiria jibu. Kuingia ufa ni kuharibika. Watahiniwa wengi walichagua jibu la ***C***, ambalo linazungumzia mabadiliko. Kubabilika kunaweza kuwa kwa uzuri au ubaya. Lakini kuingia ufa ni kuharibika au kupata matatizo, kwa hivyo jibu la swali hili lilikuwa ***A***. Maisha ya msimulizi yalianza kupata matatizo. Katika swali hili mbinu mseto ya ujuzi,ufahamu na hata matumizi inatumika.

## Swali la 35

Msimulizi hakutaka kuacha "unga" kwa sababu:

A. alikuwa amezoea uraibu wa Kamaliza
B. hakutaka kumuudhi Tamasha
C. alichelea kuondolewa kundini na wenzake
D. alichelea kudunishwa na wenzake.

**Matokeo ya swahli la 35**

| Majibu | A | B | C | *D |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 24.34 | 48.61 | 10.82 | 14.87 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 26.46 | 26.98 | 26.41 | 31.01 |

* Inaonyesha jibu sawa

Jibu la swali la *35* linapatikana katika aya ya sita pale ambapo msimulizi anasema kuwa alichelea kuitwa limbukeni na wenzake. Inaonekana kwamba katika hiyo shule pengine kulikuwa na vijana wengine waliokuwa wanatumia dawa za kulevya. Kuitwa limbukeni ni sawa na kudunishwa. Watahiniwa wengi walichagua jibu la ***B***, lakini hakuna mahali popote ambapo tunaona msimulizi akisema kwamba aliogopa kumuudhi Tamasha. Kwa hivyo jibu sawa ni ***D***. Alichelea kudunishwa na wenzake. Swali hili lilitahini mbinu ya ufahamu tu.

*Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.*

Mafunzo ya kuimarisha maadili katika jamii ni muhimu. Kinyume na hapo awali, sasa maadili ya jamii zetu yanazoroteka kwa kasi sana kiasi cha kushangaza. Mwingiliano mwingi kati ya mataifa ya Kiafrika na ya kigeni unaweza kuleta upungufu wa maadili. Watu wengi hufikiria kuwa upotovu wa maadili ndio ustaarabu ufaao. Kusifu na kuziiga nyendo mbaya huchangia upalilizi wa uozo wa tabia. Hali hii inaweza kuzifuja nchi hizi.

Ni dhahiri shahiri kuwa umaskini wa nchi umewafanya vijana kwa wazee kutamani na kuzitafuta njia za mkato za kujitajirisha. Kwa kuingiwa na tamaa nyingi, wao huanzisha miradi ya kifisadi. Watu hao hufanya juu chini kutafuta mianya ya kujipenyezea fedha. Wao hufanya haya bila ya kujali madhara yanayoletwa na hizo pilkapilka zao. Hongo huzidi kuendelezwa ili kuficha hizo njama ambazo huwa hatari kwa usalama wa nchi na watu wake.

Tamaa ikikithiri mpaka, bongo za fisadi hao hazitulii bali huenda kwa haraka isiyomithilika. Watu hujikweza wakitaka kuwafikia na kuwapita waliowatangulia kiuchumi. Mathalani, watu ambao hivi majuzi walionekana hoi ama watu wa kawaida, ghafla huonekana watu wa kuishi kitajiri huku wakijijengea majumba ya ghorofa katika mitaa ya kifahari. Kama hali hiyo ingeletwa na kushukiwa na nyota ya jaha, tungeelewa. Lakini kama utajiri huo unatokana na kufurisha mifuko kwa kuleta shoti ofisini, wakitumia wizi wa kalamu au kula mlungula, itabidi utiliwe shaka na kulaaniwa. Vijana ambao ndio wajenzi wa taifa wa leo na kesho wanapaswa kuvipuuza vitendo hivyo kwa sababu vinadhalilisha utu wa jamii.

Serikali nyingi za Kiafrika hutafuta mikakati ya kukabiliana na ufisadi ili ziimarishe maadili. Mojawapo ya hiyo mikakati ni hatua ya serikali ya kuwahimiza wananchi kujaza fomu kuonyesha jumla ya rasilimali zao. Hata hivyo, wahusika katika ufisadi hutafuta vizingiti vya kuzizuia juhudi hizo za serikali.

Ni bayana kuwa mtu hawezi kushindana na mkono mrefu wa serikali. Juhudi za kukomesha vituko vya ufisadi zimeanza kuzaa matunda. Tayari vielelezo vya kupambana na ufisadi vimeanza kujidhihirisha vyenyewe. Hivi majuzi vituko vya kujenga nyumba hafifu hapa nchini vilifuatiliwa unyounyo na wahusika kufunguliwa mashtaka; hasa baada ya watu kupoteza maisha yao na wengine kulemazwa walipoangukiwa na nyumba hizo. Kwa mfano, watu waliodai kuwa watajenga ghorofa tatu, walibadili nia na kujenga ghorofa zaidi. Walifanya hivyo baada ya kupata vibali vya pembe za chaki. Isitoshe, kwa kutaka kutajirika haraka walinunua na kuvitumia vifaa duni kinyume na kanuni za uhandisi. Mambo kama haya hujitokeza katika nchi nyingi barani Afrika. Nchi hizi sasa zimeamka na kukaza kamba katika kuupinga ufisadi huu.

Ikumbukwe kuwa ufisadi unaotokana na ukosefu wa maadili ni hatari kubwa kwa nchi yoyote ile. Mienendo kama hii hufuja nchi husika. Ni vyema kuepuka tabia hizi kama mtu aepukavyo ugonjwa wa kuambukiza.

**Swali la 47**

Upalilizi wa uozo wa tabia huendelezwa kwa:

A. kupenda na kuzifuata tabia za kifisadi
B. kufikiria tu juu ya upotovu wa maadili
C. kusifu na kuzifuata nyendo zote za kigeni
D. mwingiliano wa binadamu katika ustaarabu

**Matokeo ya swali la 47**

| Majibu | *A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 32.44 | 14.93 | 40.71 | 10.40 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 28.32 | 24.32 | 28.51 | 24.61 |

* Inaonyesha jibu sawa

Swali hili lilitahini mbinu ya matumizi.

Uozo wa tabia katika kifungu hauji kwa kufikiria tu juu ya upotovu. Huenda mtu akafikiria juu ya jambo na asifanye chochote. Nazo nyendo zote za kigeni haziwezi kuwa mbaya. Kuna zile mbaya na kuna zile nzuri. Mwingiliano wa binadamu katika ustaarabu huleta uzuri na unaweza kuleta ubaya pia. Kwa hivyo upalilizi wa uozo katika kifungu utaendelezwa tu na *A*. ***Kupenda na kuzifuata tabia za kifisadi.***

**Swali la 48**

Madhara makuu yanayoweza kupata jamii ya kifungu ni:

A. vijana kuupenda na kuuiga utamaduni wa kigeni
B. umaskini mkubwa unaorudisha nchi nyuma kiuchumi
C. watu kuingilia njama za kifisadi kwa kutaka kutajirika
D. maangamizi yanayoletwa na watu wenye njama za kifisadi

**Matokeo ya swali la 48**

| Majibu | A | B | C | D* |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 12.67 | 27.94 | 32.61 | 25.36 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 25.51 | 27.89 | 26.23 | 29.32 |

* Inaonyesha jibu sawa

Swali hili lilitahini mbinu ya tathmini na kidogo matumizi pia. Mtunzi anauliza mtahiniwa asome kifungu na kutumia ujumbe kupata jibu. Mtahiniwa pia anatakiwa atathmini ujumbe wa taarifa .

Swali linauliza juu ya madhara makuu. Neno ***makuu*** limepigiwa mstari kuonyesha msisitizo. Kutokana na vile majibu ya swali hili yanavyojitawanya ni wazi kwamba watahiniwa wengi walikuwa wanakisia jibu. Kuiga utamaduni wa kigeni hakutajwi kama madhara au kama kunaweza kuleta madhara, kama vijana hawaigi utamaduni mbaya. Umaskini katika kifungu umetajwa kama sababu ya baadhi ya watu kuingia ufisadi. Nalo jibu la ***C*** limekuwa silo kwa sababu watu kuingilia njama za kifisadi ni jambo lililojadiliwa katika kifungu ambalo linaleta madhara, nayo madhara hayo ni kama watu kuangamia kwa mfano wanapoangukiwa na nyumba zilizojengwa kifisadi. Kwa hivyo jibu hapa ni ***D. Maangamizi yanayoletwa na watu wenye njama za kifisadi.***

**Swali la 49**

Mwandishi wa taarifa hii ana msimamo kuwa:

A. ustaarabu wote wa kigeni unapotosha maadili
B. maadili yatafaulishwa na vijana na serikali husika
C. uigaji wa nyendo za kigeni unapaswa kuzuiwa
D. ujenzi wa ghorofa duni na njama za kifisadi zimezidi

**Matokeo ya swali la 49**

| **Majibu** | **A** | **B*** | **C** | **D** |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 28.56 | 20.31 | 33.42 | 16.31 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 27.20 | 28.71 | 28.25 | 24.37 |

* Inaonyesha jibu sawa

Swali hili lilitahini mbinu ya tathmini. Hapa pia, kama swali la ***48***, watahiniwa walikuwa wanakisia majibu. Mwandishi wa kifungu hakusema kuwa utamaduni wote wa kigeni ni mbaya kwa hivyo hawezi kusema uigaji wa nyendo za kigeni uzuiwe. Taarifa inazungumzia juu ya ufisadi kwa jumla kwa hivyo huo hauwezi kuwa msimamo wa mwandishi. Mwandishi yeyote akiandika lazima aonekane kutoa suluhisho ikiwa anaandika kuhusu tatizo fulani katika jamii – Naye huyu mwandishi hapa amejaribu kupendekeza suluhisho. Amezungumzia juu ya mikakati ya serikali kutafuta suluhisho na pia akataja kwamba vijana ndio wajenzi wa taifa wa leo na kesho. Kwa hivyo msimamo wake ni ***B. Maadili yatafaulishwa na vijana na serikali husika.***

## 4.2 SEHEMU YA PILI : INSHA

Mwaka wa 2007 insha ilikuwa

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu juu ya kichwa kifuatacho:

Rafiki yako amehamishwa na kujiunga na shule nyingine. Mwandikie barua ukimwelezea maendeleo yako tangu mlipoachana.

Insha hii ni ya kirafiki kwa hivyo haikuwa na mahitaji mengi kwa mtahiniwa. Mtahiniwa amepewa uwanja mpana wa kujieleza na kuandika insha yake kwa njia inayopendeza bora asitumie lugha kwa mfano isiyo ya adabu.

Yafuatayo ni maelezo ya kuonyesha jinsi alama katika viwango vine maalum zinavyofikiwa katika usahihishaji. Viwango hivi ni alama ***01-10, 11-20, 21-30, 31-40.***

### 4.2.1 Kundi la kwanza (alama 01-10)

Watahiniwa hawa, hasa wale waliotuzwa alama ***01-05***, huandika insha zao vibaya mno. Wao hutumia maneno ya Kiswahili,ya Kiingereza na lugha zao za mama yakichanganywa. Kuna baadhi wanaotumia lugha isiyoeleweka hata kidogo. Wale wanaotuzwa alama ***6-10*** huwa wameandika insha zao kwa Kiswahili kilicho na makosa mengi sana ya sarufi na tahajia. Pia mawazo yao hayatokei vizuri. Huwa pia wamepotoka kwa upande wa mada.

Powered By: www.manyamfranchise.com